THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

121/1 **KISWAHILI 1**

(Kwa watahiniwa walioko na wasiokuwa shuleni)

*Muda: Saa 3* **2007 Februari, 12 Jumatatu mchana**

---

*MAELEKEZO*

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **matano (5)** kwa kuchagua swali moja kutoka kila sehemu.
3. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
4. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.




Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (alama 20)**
**HISTORIA**

1. Maneno ya lugha nyingine yanapoingizwa katika lugha ya Kiswahili yanakidumaza Kiswahili. Jadili kauli hii.

2. Kwanini Kiunguja kiliteuliwa kuwa kipimo cha Kiswahili sanifu?

3. "Zipo nadharia potofu na zenye ukweli zinazoelezea chimbuko la Kiswahili". Thibitisha kauli hii.

**SEHEMU B (alama 20)**
**SARUFI**

4. Fafanua muundo wa silabi katika Kiswahili.

5. Kwa kutumia tungo onesha kazi **tano (5)** za mofimu "KU".

6. Tunga sentensi kutumia maneno "paa" na "tupa" na kwa kila neno litumie kama:
   (a) Kielezi.
   (b) Nomino.
   (c) Kitenzi.

**SEHEMU C (alama 20)**
**MATUMIZI**

7. Eleza maana na matumizi ya maneno yafuatayo:
   (a) Rejesta.
   (b) Lugha rasmi.
   (c) Lugha ya Taifa.
   (d) Lugha sanifu.

8. Jadili athari hasi na chanya za lugha za asili au makabila katika lugha ya Kiswahili.

9. Kwanini unaweza kumtambua mtu kutokana na mazungumzo yake? Jadili kwa kutoa mifano.

**SEHEMU D (alama 20)**
**UTUNGAJI**

10. Kwa niaba ya wanafunzi wenzako wa kidato cha sita andika hotuba yenye maneno **mia nne (400)** au yasiyopungua **mia tatu (300)** ambayo itasomwa mbele ya mgeni rasmi katika sikukuu ya mazingira ambayo itaadhimishwa hapo shuleni kwenu hivi karibuni.

11. Andika insha ya maneno yasiozidi **mia nne (400)** na yasiyopungua **mia tatu (300)** juu ya ajira za watoto.

12. Andika tangazo la nafasi ya kazi ya Afisa Utumishi Mkuu katika gazeti la "Rai". Jina na anwani ya anayetoa tangazo hilo ni:
    Mkurugenzi,
    Nguvu ya Hoja kwa Umma,
    S.L.P. 109233,
    DAR ES SALAAM.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU E (alama 20)
## UFAHAMU

13. Soma habari ifuatayo kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata.

Elimu iliyotolewa kwa vijana wa kiafrika wakati wa ukoloni haikuwa na utaratibu maalum, haikuweza kuwasaidia vijana kuelewa walichotakiwa kufanya kama wazazi wa vizazi vijavyo. Isitoshe, nafasi ya mwanamke, kila wakati ilichukuliwa kuwa siyo muhimu katika maendeleo. Wanaume ndio waliothaminiwa kama nguzo ya maendeleo katika enzi hizo. Jambo hili liliwafanya wanawake waonekane duni, watu wasiojitegemea na ambao wakati wote wanafuata matakwa ya wanaume zao kwa ujumla.

Ilikuwa vigumu kwa mwanamke kufanya jambo lolote ama kwa kutaka kufanya mabadiliko ya aina fulani ya maendeleo katika familia au jamii inayohusika bila kupata maelezo kutoka kwa wanaume ambao walijichukulia "nafasi ya mwisho" katika uamuzi wa masuala ya jamii. Kasumba hii inaendelea hadi leo, ingawa kidogo imelegezwa. Angalau wanawake wachache sasa wanaweza kuhusishwa katika utoaji wa maamuzi.

Wakati wa ukoloni mila na desturi nyingi zililenga kwenye maumbile. Wanawake walikuwa wakibaguliwa katika mambo mengi na kunyimwa vitu vingi ambavyo vingeweza kuwaweka katika nafasi nzuri kiafya na pia kuwapa uwezo mkubwa zaidi katika jukumu la malezi na uzalishaji wa mazao lililokuwa linawakabili. Ubaguzi huo pia uliongeza misuguano ya maslahi baina ya wanawake na wanaume katika nyanja za siasa, elimu na ajira. Wanaume ndio walionekana wafanyakazi thabiti, ambapo wanawake walipasishwa kuwa mama wa nyumbani huku wakiwa chini ya matakwa ya waume zao. Lakini hivi sasa, nchi nyingi duniani zimethibitisha kwamba sehemu kubwa ya maendeleo katika taifa huletwa na wanawake ambao ndio wafanyao idadi kubwa ya wananchi katika nchi nyingi.

Chini ya utawala wa wakoloni wazazi walikuwa wanahimizwa kuwaelimisha vijana wao wa kiume zaidi kuliko wale wa kike. Wavulana walikuwa wakifunzwa kwa ajili ya kujiunga na jeshi la wakoloni au kuwa manokoa katika mashamba makubwa ya katani, kahawa na chai. Kwa wasichana na wanawake wachache waliofanikiwa kupata angalau elimu kidogo, walihimizwa kujifunza masomo ambayo yanahusiana na majukumu ya shughuli za nyumbani, kama upishi, ushoni, ufumaji na kadhalika. Masomo haya kama ilivyoonekana hayakuwapatia nafasi wanawake kutoa uamuzi katika vyombo vinavyohusika juu ya masuala ya maendeleo kwa jumla.

Baada ya kupata uhuru, nchi nyingi za Afrika zimefanya juhudi kubwa kurekebisha hali hii na kuweka misingi ya usawa kati ya wanawake na wanaume. Kwa mfano nafasi zaidi za elimu ya juu zimetengewa wanawake. Idadi ya wanawake wanaohitimu katika vitivo vya vyuo vikuu katika nchi za Kiafrika inaongezeka mwaka hata mwaka. Sera za ajira pia zinatoa nafasi kwa wanawake kufanya kazi za ubingwa ambazo awali kidogo, zilikuwa amali ya wanaume tu. Mathalani, leo si muujiza au kioja tena kuona jaji, daktari, mhandisi au rubani mwanamke. Isitoshe, katika nchi nyingi za Afrika kumekuwa na ongezeko kubwa la wanawake wanaoshiriki katika masuala ya kisiasa na ya kiuchumi.

Lakini pamoja na hayo yote mintarafu ya ukombozi wa mwanamke, vikuku vingine katika sera za ajira vinabidi vifunguliwe. Kwa mfano, bado idadi kubwa ya wanawake hasa viwandani, si watumishi wa kudumu, hivyo hulipwa mishahara midogo, hawaongezwi ujuzi wao kwa kusomeshwa na pia si rahisi kwao kupandishwa cheo. Kutokana na hali hii, wanawake wengi wamekuwa wakifanya kazi ambazo hazitoi nafasi za kujiendeleza.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## MASWALI

(a) Eleza maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu cha habari ulichosoma:

(i) Msuguano.
(ii) Matakwa.
(iii) Manokoa.
(iv) Msemaji wa mwisho.
(v) Sera ya ajira.
(vi) Maendeleo.
(vii) Vikuku.
(viii) Kasumba.
(ix) Maumbile.
(x) Kupasishwa.

(b) Andika kichwa cha habari hii.

(c) Kwanini wazazi walipendekeza kusomesha vijana wa kiume?

(d) Jadili jitihada zilizofanywa na serikali ili kuinua hadhi ya wanawake.

(e) Andika ufupisho wa habari hii usiopungua maneno **mia moja** (**100**) na usiozidi maneno **mia moja na hamsini (150)**.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org